
# Shule Nzuri ni Ipi?

Kufikiria kupita vikwazo vya leo ili kujenga kesho iliyobora



*Dipak Naker*

Raising Voices

Shule Nzuri ni Ipi?

**Imagining beyond the limits of today to create a better tomorrow**

By Dipak Naker

Copyright © 2007 Raising Voices
All rights reserved.

ISBN: 9970-893-09-5

All photographs © Heidi Jo Brady and printed by permission of the photographer for this publication only.

Photography: Heidi Jo Brady (hojos@earthlink.net)
Editing: Stephanie Sauvé (stephanie@stephaniesauve.com)
Design: Samson Mwaka (mwakasw@yahoo.co.uk)

**Raising Voices**
16 Tufnell Drive, Kamwokya
PO Box 6770
Kampala, Uganda
Tel: +256 41 4531186
Fax: +256 41 4531249
Email: info@raisingvoices.org
Website: www.raisingvoices.org

# Shule Nzuri ni Ipi?

## Kufikiria kupita vikwazo vya leo ili kujenga kesho iliyobora

*Dipak Naker*

Raising Voices

Kwa msaada wa The Ford Foundation

# Shukrani

Mawazo yaliyowasilishwa katika chapisho hili yameendelezwa kwa pamoja na washirika kutoka sehemu mbali mbali za Afrika waliokusanyika Nairobi kujadili uzoefu wao wa kubuni shule salama zaidi. Tulichapisha matokeo ya moja kwa moja ya mkutano huo katika Ubunifu wa Shule Salama: Mambo tuliyojifunza; Mikakati kwa ajili ya Utendaji (angalia www.raisingvoice.org). Hata hivyo, uzoefu na ujuzi wa kundi hili uliamsha majadiliano mapana, tafakuri na msukumo ambavyo vimekuwa nguvu ya msingi katika uandishi wa chapisho hili. Tunatoa shukrani zetu za pekee kwa wote walioshiriki, hasa Carla Sutherland wa Ford Foundation aliyebuni uwezekano wa mchakato kama huu na kuunga mkono.

TMsisitizo katika chapisho hili wa kushirikisha eneo la fikra bunifu ili kuwa na shule bora umeletwa na Rakesh Rajani wa HakiElimu. Ushawishi na uwezo wake wa kuwasilisha mawazo mazito kwa hisia unaendelea kutuvuta na kututia nguvu sisi sote tunaofanya kazi kubuni shule bora.

Shukrani zetu pia tunazitoa kwa watoto wengi wa Uganda na waalimu waliotufundisha mengi kuhusu uthabiti, ujasiri na fikra bunifu. Bila michango yao, mawazo haya yangekosa uharaka na uhalisi katika vitendo. Hasa hasa tunapenda kuwatambua waalimu wenye dira na wanafunzi wenye mwazo mapya wa Shule ya Sekondari Mulango, na Shule ya Msingi ya Mt. Petro-Kanyanya, Uganda ambao wameshaanza kubuni shule bora kwa jamii zao. Msimamo wao na utayari wa kuchangia uzoefu wao umeshawishi sana mengi ya yanayowasilishwa katika chapisho hili ili uweze kuyatafakari.

Kupitia sera ya upatikanaji wa elimu kwa wote, tunatengeneza nafasi kwa watoto wengi kuendeleza ujuzi utakaoboresha maisha yao. Hii ni hatua kubwa kwenda mbele ya fursa kwa watoto, ambao kwa muda mrefu sana, wamekaa pembezoni mwa jamii yetu. Hata hivyo, wakati tunafungua milango ya shule zetu kwa watoto wengi zaidi, ubora wa elimu katika shule hizi huaathirika. Tusipohakikisha kuwa maisha ya shule yanakuwa na maana na kukidhi matarajio ya wanafunzi, jitihada zetu zitakuwa ni ishara tupu.

Pamoja na kupanua mwelekeo wetu katika kuwezesha upatikanaji wa elimu tunahitaji pia kujali ubora wa elimu hiyo. Katika kufanya hivyo, tutaibua maswali mapya na changamoto zinazostahili umakini na majadiliano. Kuendeleza majadiliano haya, chapisho hili linachangia mawazo na mitazamo kuhusu nini sifa za shule bora na jinsi gani tunaweza kubuni kwa pamoja shule bora kwa watoto wetu.





Maendeleo yoyote makubwa yametokana na ujasiri mpya wa ubunifu.

*John Dewey*

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| **Chapisho hili ni kwa ajili ya nani?** | ii |
| **Utangulizi** | 1 |
| **Sura ya 1** \| Kufikiria Shule Bora | 5 |
| Shule zetu hivi sasa | 5 |
| Kumwelimisha mtoto kwa ujumla wake | 8 |
| Sifa za shule bora | 10 |
| Itahitaji nini kutengeneza shule bora? | 11 |
| **Sura ya 2** \|Kuendeleza Utambuzi katika Shule Bora | 13 |
| Stadi za utambuzi na hatua za kujifunza | 14 |
| Methodolojia yetu ya kufundishia sasa | 16 |
| Methodolojia ya kufundishia ya shule bora | 18 |
| **Sura ya 3** \| Uendelezwaji wa Kijamii katika Shule Bora | 21 |
| Heshima/Hadhi | 23 |
| Sauti | 26 |
| Nidhamu Chanya | 28 |
| **Sura ya 4** \| Uendelezwaji wa Maadili katika Shule Bora | 31 |
| Uhusiano kimaadili | 34 |
| Viwango | 35 |
| Sera stahili iliyoandikwa | 36 |
| Utawala unaowajibika | 38 |
| Ushiriki wa jamii | 39 |
| **Maneno ya Mwisho** | 41 |
| **Maelezo** | 42 |
| **Marejeo yaliyoshauriwa** | 43 |

# Chapisho Hili ni kwa Ajili ya Nani?

Hili chapisho ni kwa ajili ya mtu yeyote mwenye ushawishi kuhusu watoto wanavyopata elimu katika shule zetu. Linajaribu kuwafikia watawala wa shule, waalimu, watungasera na wanaharakati wanaotambua mahitaji ya kuboresha jinsi tunavyotoa elimu. Linalenga kuwafahamisha na kuwahamasisha wale watu wanaotambua shule kama sehemu yetu ya matumaini, ya uwekezaji wetu wa baadaye na ahadi/wajibu wetu kwa watoto leo. Kwa kifupi, chapisho hili linazungumza na kila mmoja mwenye wajibu katika kubuni shule bora.

**Chapisho hili ni mjadala wa mawazo na siyo mwongozo wa utekelezaji. Linawasilisha hoja na michango inayohitaji kufikiriwa sasa wakati tunatengeneza mustakabali. Kama mdau mwenye maslahi na mwenye ushawishi, maamuzi yako yanaweza kuathiri jinsi shule zetu zitakavyoendelea katika miaka ijayo. Kwahiyo hili chapisho linawasilisha mitazamo na taarifa inayoweza kusaidia kufikri na kuchagua.**

Matumaini yetu ni kwamba, jinsi unavyosoma hili chapisho, utauliza maswali ya kina zaidi kuhusu jinsi tunavyotoa elimu na itakavyoweza kuwa tofauti na bora. Kwa kuwekeza ushawishi wako, rasilimali na ubunifu katika kutekeleza baadhi ya mawazo yafuatayo unaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa sana maisha ya watoto wengi – pamoja na maisha yatakayoguswa na maamuzi yatakayofanywa na watoto hawa pale watakapokuwa viongozi wetu baadaye.

*Chapisho hili huzungumza na kila mmoja mwenye jukumu katika ujenzi wa shule bora.*



*Kama tukisaliti mategemeo yao watatoka kwenye mfumo wakiwa na ndoto zilizozimwa na matumaini yaliyoachwa. Tutakukuwa pabaya zaidi kuliko tulipoanzia; matumaini yaliyopotea ni hali mbaya sana ya akili.*

# Utangulizi

*Nchi nyingi za Kiafrika zimewekeza kiasi cha fedha ambacho hakijawahi kutokea kuwezesha upatikaji wa elimu yamsingikwawote.Nchinyingi, kama Uganda na Tanzania, zilitangaza kuwa wako mbele ya ratiba iliyokubaliwa, na zingine zinahimiza upatikanaji wa elimu ya sekondari kwa wote.*

Hata hivyo wakati tunatathmini uzoefu wa sera ya elimu kwa wote, tunagundua kuwa wanafunzi wengi wanachukua kwa hamu fursa hii mpya wanaishiwa na hamu hiyo mara moja baada ya kuona hali wanayoikuta shuleni: vurugu, uhaba wa miundombinu, vikwazo kwenye fikra bunifu na mipaka katika fursa za kujieleza, miongoni mwa mengine. Kwa haraka, tunagundua kuwa fursa ya kuingia shule ni hatua ya mwanzo tu ya kufanya elimu iwezekane kwa mamilioni ya watoto. Wanayoyakuta wanapoingia shule huamua kama watoto wetu watahitimu wakiwa na uwezo wanaouhitaji au la.

Kuwekeza miaka muhimu ya maisha ya mtu katika elimu ni msimamo wa kipekee kwa mtoto na familia; nguvu kazi ni bidhaa ya thamani sana katika mazingira yasiyokuwa na rasilimali. Kuchukua hatua hiyo kwa faida inayotarajiwa baadaye ni kitendo cha matumaini – ni matamanio makubwa ya wazazi ya kujitoa katika hali ya dhiki. Kama tukisaliti mategemeo ya wanafunzi na wazazi wao, watapiga kura kwa miguu yao, kama walivyofanya katika maeneo mengi. watatoka kwenye mfumo wakiwa na ndoto zilizozimwa na matumaini yaliyoachwa. Tutakukuwa pabaya zaidi kuliko tulipoanzia; matumaini yaliyopotea ni hali mbaya sana ya akili.

Kama tusipoongezea uwekezaji wetu wa upatikanaji wa elimu kwa kuhakikisha pia ubora wke, tutadhoofisha sana juhudi zetu. Kama tusipochunguza swali, shule bora ni nini? Na kujibu kwa ubunifu, wanafunzi wetu watashindwa kufanikiwa. Watabaki wamefungiwa katika hali ya hasara, bila uwezo wa kushindana; watakuwa wakitumika katika uchumi na utamaduni wa utandawazi. Katika mazungumzo ya kidunia ya fikra na ushawishi watalazimishwa kuwa wakimya, kufuata uongozi wa wengine, kujihisi kuelemewa kwa kutokuwa na mamlaka na kutokufaa kwao. Kama tukiendelea kudumaza vichwa vyao na kuwatia ganzi ya usikivu na utiifu, badala ya kuwapatia ujuzi na kuwapa nyenzo wanazohitaji kuwafanya wabunifu na watu wa fikra, watabaki kama tulivyo leo: wenye mapungufu, tusiotimilika, tusiowashindani, na, kama kundi, maskini kiuchumi.

Lakini siyo lazima iwe hivyo. Maamuzi tunayofanya leo yanaweza kuwasaidia wanafunzi kuwa watetezi wa mawazo yao wenyewe, pamoja na mitazamo na misimamo yao. Wanafunzi wanahitaji kuwa na ufahamu na ujuzi unaoweza kutumika katika mazingira yanayobadilika. Wanahitaji uhodari na imani ya kuamini silika zao. Wanahitaji nidhamu ya kufikia kilele cha uwezo wao. Kama tukichagua kubuni shule zinazoendeleza uwezi huu, tutakuwa tunawaandaa watu watakaokuwa injini za utamaduni na uchumi wetu, watakaopanua uwezekano wao wa kuleta nguvu na hamasa za vipaumbele vyao kuvuta usikivu wa dunia.

*Tunahitaji kujiuliza, katika dunia ya leo elimu bora ni nini? Na ni aina gani ya shule itaitoa? Aina gani ya shule itawaandaa wanafunzi wetu kufanikiwa katika mazingira haya mapya? Tunahitaji kuyafanya maswali haya kuwa vipaumbele vya haraka, kuyapa usikivu wote wa ubunifu wetu.*



*Kikwazo chetu kikubwa katika kuwa na shule bora si ukosefu wa nia bali upungufu wa fikra bunifu.*

# Sura ya 1 | Kubuni Shule Bora

Kubuni ni uwezo wa kuona kitu ambacho bado hakipo. Ni uwezo wa kutengeneza katika fikra zetu njia mpya za kutatua matatizo ya zamani. Kikwazo chetu kikubwa katika kuwa na shule bora si ukosefu wa nia bali upungufu wa fikra bunifu. Tumekubali kubaki katika uchovu wa fikra, kushindwa kusonga mbele kuvuka mipaka iliyowekwa na uzoefu wetu. Ni muda wa kufikiri zaidi ya mipaka ya uzoefu wetu na kubuni shule inayokidhi mahitaji ya sasa ya watoto.

## Shule zetu hivi sasa

Kwanini idadi kubwa ya watoto waliotamani sana nafasi ya kujifunza sasa wanaiacha ndoto hiyo?[1]

Shule zetu zimejikita katika mawazo yaliyokuwa sahihi kwa wakati uliopita. Wengi wetu tumezoea kufikiri kuwa shule ni sehemu ambayo watoto wanajifunza kufaulu mitihani kwa kukariri anachokiandika mwalimu ubaoni. Tunatarajia watoto kuwatii waalimu wao na kukaa kimya mpaka watakaposemeshwa. Tunalenga kuwajengea hofu ya kuvunja sheria na madhara yake. Shule zetu zinajiendesha kwa kuwatisha na kuwajengea watoto nidhamu ya woga ili wafanye yanayotarajiwa kutoka kwao.

Tunapima shule kwa kuzingatia vipimo finyu, kama matokeo ya mitihani ya wanafunzi. Ili mradi shule inawalazimisha wanafunzi wake kufaulu mitihani yao, tunakubali kuwa shule hiyo imetimiza wajibu wake. Tumekubali mtazamo huu finyu kuhusu maana ya shule bora, kwa sababu mpaka hivi karibuni, katika nchi nyingi zinazoendelea, kuwa tu na fursa ya kwenda shule ilionekana kama bahati.

Waalimu wengi waliosoma katika shule kama hizi watauliza, kuna ubaya gani kwa shule kufundisha nidhamu ya utii na usikivu kwa watoto? Hizi siyo sifa muhimu tunazotaka watoto wetu kuwa nazo? Hatuhitaji watoto wetu kujifunza mila za siku nyingi za kuwaheshima wakubwa zao na kuwatii walio juu yao? Hofu na kuona haya siyo zana zinazofaa katika kuwafundisha watoto tabia nzuri?

Uhalisia ni kwamba mfumo huu wa kufundisha umeshindwa kufanya kazi.[1] Kila mmoja anakubali kuwa watu wazima wana nafasi muhimu katika kuelekeza makuzi ya watoto. Hata hivyo mbinu zetu za kufikia lengo hilo zinakosa uaminifu. Wengi wa watoto wetu wanatoka katika shule zetu wakiwa na kiwango kidogo sana cha uwezo wanaohitaji ili kufanikiwa katika uchumi wa kisasa. Zaidi ya hayo, tunagundua kuwa kuwatisha, kuwafundisha kuona aibu na kuwafedhehesha watoto hakuwasaidii kujifunza stadi mpya. Inachofanya ni kuzuia uwezo wao.

Muafaka wa ulimwengu wote unaanza kujitokeza (angalia Taarifa ya Dunia Juu ya Matumizi ya Ukatili Dhidi ya Watoto) kuwa mkakati tunaotumia sasa kuwaelimisha watoto haufai kwa sababu zifuatazo:

- Unalazimisha utiifu kwa muda mfupi na kujenga chuki na uasi kwa muda mrefu.

- Watoto wengi wanashindwa kuhimili msongo wa kisaikolojia wa hofu, aibu na, kwa hiyo, mara nyingi huficha hisia zao. Uzoefu huu huwafanya wao kurudi nyuma na kuacha kutoa mawazo yao ya kipekee kwa jamii zao.

- Watoto watiifu na waoga wanajifunza kuendana na njia zilizozoeleka za kuwa na za kufikiri na, kwa hiyo, hawaendelezi stadi za lazima kuleta majibu muafaka kwa matatizo mapya.

- Kuwazuia watoto kujitambua wao ni akina nani huwanyima haki zao za msingi za kuwa huru na za utu, walizohakikishiwa katika katiba za nchi nyingi za Kiafrika na kuridhiwa na serikali nyingi za Kiafrika katika mikataba ya kimataifa.

Kwa sababu hizi na zinginezo, ni muhimu kubuni njia mpya za kuwaelimisha watoto wetu.

Kama ukiwauliza watoto kuhusu hali hii, wengi wo watakuambia kuwa shule si mahala pa kufurahisha kwao. Shule kama tunavyozielewa leo hazimlengi mtoto. Zina uhaba wa shughuli, mbinu na mazingira yanayoamsha ubunifu na uwezo wa mawazo huru ambao watoto wa leo wanahitaji. Wanavumilia hali zinazowadhalilisha watoto na kuruhusu ukatili dhidi ya watoto kufanyika bila wahusika kuadhibiwa.

Licha ya sera za taifa na misimamo iliyotangazwa ya kuwalinda watoto, wanafunzi wamekuwa wanapokea vipigo, adhabu zinazowashushia hadhi, unyanyasaji wa kijinsia, uonevu na udhalilishaji. Katika utafiti uliofanywa chini ya UNICEF katika nchi kumi na moja za Afrika kusini mwa Sahara, ofisi za nchi saba kati ya kumi na moja ziliorodhesha ukatili shuleni kama mojawapo ya vipaumbele vikubwa vitatu vya kushughulikiwa2. Katika uchunguzi uliofanywa Uganda , zaidi ya asilimia sitini ya wanafunzi walishiriki katika utafiti walisema kuwa kwa kawaida wanakumbana na vitendo vya ukatili shuleni, na kutokana na ushahidi uliopo, hali siyo tofauti katika nchi nyingine za Kiafrika.

Je, huku siyo kuwa tunashindwa, licha ya kudhani tumefanikiwa kuwaelimisha watoto wetu? Kutokana na mahitaji yetu ya haraka ya watu wabunifu na wenye fikra, huu uhamaji wa wataalam ni endelevu?

*Kila mmoja anakubali kuwa watu wazima wana nafasi muhimu katika kuelekeza makuzi ya watoto. Hata hivyo mbinu zetu za kufikia lengo hilo zinakosa uaminifu.*

# Kumwelimisha Mtoto kwa Ujumla Wake


Shule bora inalenga kumsaidia mtoto kujifunza kwa kuzingatia mahitaji ya maendeleo ya mtoto kwa ujumla. Inakuza utambuzi, ukuaji kijamii na kimaadili wa mtoto.

**Kukuza utambuzi:** Kupitia mbinu ya kufundishia iliyojikita kwa mwanafunzi na ujenzi wa stadi, shule bora huendeleza uwezo wa wanafunzi kuchambua na kutengeneza taarifa kwa ufanisi. Inajikita katika kuwafundisha watoto namna ya kujifunza kuliko namna ya kukariri taarifa.

**Ukuaji kijamii:** Kupitia mahusiano ya heshima, ushauri na uelekezwaji makini, shule bora hukuza watoto kujiamini na uwezo wa kuamini maamuzi yao wenyewe. Inawapa watoto nafasi ya kutambua uwezo wao na kuamua vipaumbele vyao. Shule bora huendeleza mazingira ambamo watoto wanahisi kukubalika, kuthaminiwa na kujifunza wajibu wao katika kuhusiana na wengine.

**Ukuaji kimaadili:** Kupitia miundo ya kidemokrasia na uwajibikaji, kuwa mfano mzuri wa kuigwa, na sera endelevu, shule bora huendeleza uwezo wa watoto kushiriki kutekeleza sera hizo na kuonyesha hali ya kujali kama raia. Shule bora hupalilia viwango dhahiri vya maadili ambavyo huwasaidia watoto kujijengea ndani mwao mfumo wa maadili kwa maisha yao yote.

Shule bora inatambua kuwa kukua kwa utambuzi wa watoto kunategemea uwepo wa mazingira yanayowawezesha kijamii na kimaadili shuleni. Kujifunza kiufanisi kutatokea tu pale ambapo mtoto amefundishwa stadi anuai za utambuzi zinazohitajika kupitia ngazi mbalimbali za mchakato wa kujifunza, zikiwepo: kushika taarifa, kuchambua maana yake, kuchunguza thamani yake na kuitumia. Uendelezwaji wa stadi hizi unahitaji mtoto kuhisi kukubalika, kulindwa na kuheshimika, pia kujihisi kuwa sehemu ya mazingira ya kujifunzia. Mazingira haya ya kijamii yanaweza kukuzwa kwa kulea ukuaji kimaadili kwa kujenga mahusiano yenye huruma, kuwashauri watoto, kuwapa mazingira yenye mpagilio na kuonyesha viwango wazi ambavyo kila mmoja anavifuata katika mazingira hayo (tazama mchoro katika ukurasa unaofuata). Ni athari za ushirikiano wa vigezo vyote hivi vinayozalisha watu wenye fikra bunifu na wanaopata majibu ya matatizo kwa ubunifu. Sura zinazofuata zinajadili mawazo haya kwa undani zaidi.




Kujifunza ni matokeo ya mwingiliano uliochangamana baina ya stadi za mwanafunzi kutengeneza taarifa na mazingira ya kijamii na kimaadili ya shule.

# Sifa za shule bora

**Shule bora hutengeneza uzoefu, mazingira na mahusiano yanayowawezesha watoto kufanikiwa na kugundua uwezo wao kamili.** Inawaingiza watoto katika utamaduni unaothamini utu wao, kuendeleza nafsi zao na kufungulia akili zao. Shule bora ni mahali ambapo watoto hutambua hisia zao. Ni mahali ambapo watoto huendeleza kujitambua zaidi, kujiamini, kujihakikishia na pia kuamini kuwa wanaweza kutoa mchango unaofaa kwa jamii yao na nchi.

**Shule bora inaongozwa na waalimu wenye dira wanaotambua kuwa elimu ni zaidi ya kinachotokea darasani.** Inaongozwa na watu wenye dira ya kuwa na jamii bora na wanaoelewa nafasi ya shule katika kuamua maadili yanayoingia katika jamii yao.

**Shule bora hujiendesha kulingana na utume wa pamoja na maadili na viwango dhahiri.** Inatoa mawazo endelevu kuhusu haki za kijamii, haki za binadamu, na matarajio makubwa ya taifa. Inajiona kama hazina ya matumaini, ambapo wanajamii hujitambua na kulea vizuri nafsi zao.

**Shule bora ina sera muafaka na utaratibu wa kiutendaji wenye uaminifu kwa utume wa shule.** Inabuni utaratibu na miundo inayorasimisha maadili ambayo shule huamini. Inaendeshwa kwa ufanisi na kwa kanuni imara zinazoongoza mchakato wa kufanya maamuzi ya siku hadi siku. Shule bora hujumuisha na hutoa nafasi kwa wadau wote kushiriki.

**Shule bora hutoa mafunzo kama suala muhimu la maisha yote.** Inawezesha ukuaji wa watoto na kuwasaidia kugundua mfumo wa maadili utakaokuwa dira yao duniani. Shule bora ni tumaini letu la pamoja la kujenga taifa lenye huruma, lenye kufikiri na lenye busara.

# Itahitaji nini kubuni shule bora?

Kubuni shule bora kutahitaji rasilimali fedha – sehemu kubwa ya bajeti ya taifa, itakayotumiwa kimkakati zaidi. Itahitaji utashi wa kisiasa utakaohakikisha kuwa sera ya elimu kwa wote inakua kuakisi vipaumbele vya kina vya elimu na uelewa uliopanuka kuhusu wajibu wa serikali na watoa elimu.

Hata hivyo, viungo muhimu sana vya kuongeza ubora wa shule zetu vitakuwa ni nguvu, msimamo na dira ya mtu mmoja mmoja. Kutahitajika watoa elimu mmoja mmoja wenye hisia za kweli kuhusu mawazo haya na wanaoyatekeleza. kutahitajika waalimu, wazazi, wanafunzi na wafanya maamuzi wa ngazi ya jamii wanaoyazungumzia mafanikio yao kwa ustadi na kuwashawishi watoa elimu wengine kuyapa mawazo haya uzito unaostahili.

Kubuni shule bora, popote pale ulipo, itakuhitaji kuchuku hatua ya kwanza. Jiulize mwenyewe, nitaifanyaje? Nitachukua nafasi gani kuhakikisha hili linatokea katika shule yangu au katika shule iliyopo ndani ya jamii yangu?

*Viungo muhimu sana vya kuongeza ubora wa shule zetu vitakuwa ni nguvu, msimamo na dira ya mtu mmoja mmoja.*



*Mbinu ya kufundishia tunayoitumia na mahusiano tunayoitumia nayo, lazima iwatie moyo watoto kwa makusudi ili kupata na kuendeleza stadi za utambuzi wanazozihitaji.*

# Sura ya 2 | Kuendeleza Utambuzi katika Shule Bora

Sababu kubwa ya wazazi kuwapeleka watoto shule ni kuhakikisha kuwa wanapata elimu. Kwa watu wazima wengi "kupata elimu" kunamaanisha kuwa na uwezo wa kujua kusoma na kuandika, na pia kupata faida zitokanazo na kujua kusoma na kuandika. Kujifunza katika muktadha huu kunawahitaji watoto kufanya mazoezi ya namna mbalimbali za kutengeneza taarifa na kuendeleza uwezo wa kuchagua tabia ambazo watu wazima wanatarajia watoto waliosoma kuwa nazo. Hizi zinaitwa kwa ujumla wake stadi za utambuzi; kujifunza ni, kwa kweli, kuwapo pamoja kwa stadi anuai za utambuzi.

Vitu vingi vinaathiri uwezo wa mtoto kupata na kuendeleza stadi za utambuzi, vikiwemo mazingira ya nje ya shule na hali ya lishe ya mtoto. Mtoto aliyeingizwa katika mazingira mabovu atajitahidi sana kuwa na nidhamu inayotakiwa ili kuwa makini. Mtoto mwenye njaa na aliyeathirika na uhaba wa lishe anaweza kuwa na mipaka ya kuwekeza katika mchakato wa kujifunza. Matatizo haya makubwa ya kisiasa lazima yafanyiwe kazi, kwa mikakati ambayo inaweza kuwa nje ya uwezo wa waalimu na watawala.

Hata hivyo, vitu vingine ambavyo vimo ndani ya udhibiti wa moja kwa moja wa shule vinaweza kusaidia uwezo wa watoto kujifunza, navyo ni, jinsi tunavyofundisha na jinsi tunavyohusiana na watoto. Tunajua kuwa kujifunza ni kuunganika kwa stadi mbalimbali za utambuzi, ambazo zinaweza kufundishwa na kuimarishwa kwa mazoezi. Kwahiyo mbinu ya kufundishia tunayoitumia na mahusiano tunayoitumia nayo, lazima iwatie moyo watoto kwa makusudi ili kupata na kuendeleza stadi za utambuzi wanazozihitaji: uwezo wa kushika, kuchambua, kuchunguza na kutumia taarifa.

## Stadi za utambuzi na hatua za kujifunza

Kulinganisha kwa ufanisi na kujadili mbinu ya sasa ya kufundishia na mbadala wake, lazima kwanza tujenge msingi wa ulinganishaji wetu, mfumo wa kuelewa uhusiano hasa kati ya kujifunza na stadi za utambuzi.

Kujifunza ni mchakato unaojigawa katika hatua nne . Ili kuwa na wanafunzi wenye ufanisi, watoto lazima waendeleze aina anuai za stadi za utambuzi zinazohitajika kupita hatua zote nne za kujifunza.

### Hatua 1: Kukamata taarifa.

Hatua hii huhitaji mwanafunzi kuwa makini na kuhifadhi kwenye kumbukumbu kiasi kikubwa cha taarifa. Wanafunzi wanaoweza kukamata taarifa kwa haraka wamejenga stadi za kuwa makini na kulenga kile anachoelezwa. Pia wamejenga stadi za kuaminika na zenye ufanisi za kukariri taarifa.

### Hatua 2: Kuchambua usahihi wa taarifa.

Hatua hii inahitaji mwanafunzi kulinganisha taarifa na taarifa zingine ambazo tayari wanazijua na kupima kama ni sahihi na zina maana. Wanafunzi wanaoweza kuchambua taarifa kwa ufanisi wamejifunza kutumia stadi za kufikri kimantiki na wana uwezo wa kuhifadhi taarifa sahihi katika ufahamu wao wa karibu.


### Hatua 3: Kuchunguza maana ya taarifa.

Hatua hii inahusisha kufuatilia taarifa mpaka kwenye hitimisho na kufanya maamuzi kuhusiana na usahihi wake au manufaa yake. Wanafunzi wanaoweza kufanya maamuzi mazuri na yenye sababu wamejenga stadi na kujinoa silika zinazowawezesha kufanya maamuzi yaliyokomaa.

### Hatua 4: Kutumia taarifa.

Hatua hii inahusisha kutengeneza maana ya ujumla au kanuni za jumla kutokana na taarifa na kuzitumia katika mazingira mengine. Wanafunzi wanaoweza kutumia kile walichojifunza wanakuwa na stadi za kusanifu taarifa, kujumuisha kutokana na hali mahususi na kutafakari muonekano mwingine wa kanuni ya jumla.

# Hatua za Kijifunza




Kujifunza ni mchakato unaohitaji mwanafunzi kusafiri kutoka hatua ya 1 mpaka hatua ya 4. Wakati wa safari hii, mwanafunzi anahitaji stadi za utambuzi na nidhamu binafsi kupita hatua hizi nne.

# Mbinu yetu ya sasa ya kufundishia

Mbinu yetu ya sasa ya kufundishia imejikita katika dhana zifuatazo:

- Wanafunzi wanajifunza kwa kukariri taarifa walizopewa. Kwahiyo, mwalimu anategemea unakili mzuri wa taarifa nyingi na kukumbuka kwa usahihi.
- Jinsi wanavyojisikia wanafunzi wakati wanajifunza taarifa hizo siyo muhimu. Kwahiyo, mwalimu analenga kutoa taarifa badala ya kutaka kujua jinsi taarifa inavyopokelewa.
- Kushindwa kuelewa taarifa kama ilivyoelezwa na mwalimu hutokana na kukosekana kwa juhudi kwa upande wa mwanafunzi. Kwahiyo, mwalimu anajisikia kudhalilishwa binafsi pale mwanafunzi anaposhindwa kuelewa.
- Woga na aibu itawahamasisha kufanya jitihada zinazotakiwa na kuepuka makosa. Kwahiyo, mwalimu anatumia adhabu ya viboko ili kulazimisha mamlaka yake darasani.
- Kupata maksi za chini kwenye mtihani ni kufeli kwa mwanafunzi, siyo mwalimu. Kwahiyo, mwalimu anawaadhibu wanafunzi pale wanapofeli mtihani.

Tunavyozidi kufahamu jinsi watu wanavyojifunza, tunatambua kuwa nyingi kati ya dhana hizi hazina manufaa au ni dhahiri kwamba siyo sahihi. Mbinu yetu ya sasa ya kufundishia inakwamisha mchakato wa kujifunza kwa namna kuu mbili:

1. **Mbinu yetu ya sasa ya kufundishia kimsingi inalenga tu kwenye hatua ya kwanza ya kujifunza, kwahiyo hufupisha mchakato wa kujifunza.** Kujifunza kwa ufanisi kunahitaji zaidi ya kazi ya kukariri; kunahitaji marudio, mazoezi na mwongozo wa namna ya kuunganisha taarifa na taarifa ambayo tumeshajifunza. Kujifunza kwa ufanisi kunahusisha kuchunguza, kuuliza maswali na kuona taarifa na maana zake katika namna mbalimbali mpya-yote kwa mifano kutoka kwa watu wazima wanaoaminiwa.

2. **Mbinu yetu ya sasa ya kufundishia inatumia vitisho vya viboko au ufedheheshwaji wa wazi kuwafanya wanafunzi wasome na watii, kwahiyo hujenga msongo wa saikolojia darasani.** Katika aina hii ya mazingira ya kujifunza, wanafunzi wanajirudisha katika usalama wa kukaa kimya na matokeo yake ni kukwamisha stadi zao za utambuzi. Zaidi ya hayo, ukosefu wa kutiwa moyo na kukosolewa mara zote – ikichanganywa na woga na wasiwasi – inawezekana ikashusha sana hali ya kujiamini katika uwezo wao na kunaweza kusababisha kujijengea imani kuwa wao ni wanafunzi wazito kujifunza. Ikishajengeka, imani hii inaweza kudumu maisha yao yote.

*Mbinu yetu ya sasa ya kufundishia inakwamisha uwezo wa watoto kupita mchakato wa kujifunza.*

## Mbinu ya kufundishia ya shule bora

Mbinu ya kufundishia ya shule bora imejikita katika dhana zifuatazo:

- Wanafunza wanajifunza kwa kuendelea taratibu kupitia hatua zote nne za mchakato wa kujifunza, kila hatua ikifanya kazi kwa kuunganika na nyingine. Hii inamaanisha kuwa kujifunza kunakuwa kwa undani zaidi kwa kila hatua ambayo mwanafunzi anaipitia. Kwahiyo, mwalimu mara zote anawatia moyo na kuwasaidia wanafunzi kujenga stadi za utambuzi kuweza kupita hatua zote.

- Msongo wa mazingira ya nje (madarasa chakavu, vyoo visivyo visafi) na mazingira ya kisaikoloji (woga, wasiwasi, aibu) vinaathiri kwa undani sana upatikanaji wa stadi za utambuzi. Kwahiyo, mwalimu anajenga eneo salama kujifunzia.

- Wanafunzi wote wanataka kujifunza. Kushindwa kufanya hivyo inaakisi mwanafunzi kushindwa kuona usahihi wa taarifa anayopewa. Kwahiyo ni wajibu wa pande zote mwalimu na mwanafunzi kufanya taarifa iwe na maana na kuiunganisha na maana pana katika mtazamo wa mtoto.

- Kujifunza kutahitaji kubahatisha, kunakoendana na kutiwa moyo na uvumilivu kutoka kwa mwalimu.

- Kupata maksi za chini katika mtihani inawezekana ikawa inaakisi uhusiano baina ya mwalimu na mwanafunzi na mazingira ya kujifunzia badala uwezo wa mtoto peke yake.

*Mbinu ya kufundishia ya shule bora imejikita katika kuwawezesha watoto kupita mchakato wa kujifunza.*

Mbinu ya kufundishia ya shule bora inasaidia kujifunza katika njia kuu mbili:

1. **Mbinu ya kufundishia ya shule bora inatoa nafasi kwa watoto kujenga stadi zote za utambuzi wanazohitaji ili kuwa wanafunzi wenye ufanisi.** Kinachotokea shuleni, ndani na nje ya chumba cha darasa, kinaonekana kwa ujumla kuwa kinachangia ujenzi wa utambuzi wa watoto.




2. **Mbinu ya kufundishia ya shule bora inahusisha kuwasaidia watoto kuelewa dunia inayowazunguka, kupima taarifa wanayopewa na kufanya maamuzi ya maana yake.** Inalenga kuwachochea watu hawa wadogo kuuliza maswali na kutokuogopa kufanya makosa. Inahusu kuwajengea watoto kujiamini katika kujifunza stadi mpya na kujali jinsi watoto wanavyojisikia katika mchakato wote wa kujifunza.



*Ni kupitia mahusiano yetu ya kijamii na jinsi tunavyohisi ndani yake ndiyo tunajenga ujamii wetu.*

# Sura ya 3: | Ukuaji wa Kijamii katika Shule Bora

Kila mmoja wetu anagundua kuwa jinsi tulivyo kunategemea mahusiano ya kijamii tuliyonayo na wengine. Tunajifunza kujaribu kwa njia tofauti za tabia, kuelezea fikra zetu, kuchunguza hisia na kufanyia mazoezi stadi katika mahusiano yetu na wengine. Ni kupitia majaribio haya tunajenga nafsi zetu taratibu na namna tunavyozielezea katika jamii zetu. Hii inaitwa ukuaji wetu wa kijamii.

Ukuaji wa kijamii wa watoto ni mchakato unaohitaji uangalifu mkubwa unaotegemea jinsi mazingira yao yanavyoitikia kwa baadhi ya mahitaji yao ya msingi[4].


- Watoto wanahitaji kukubalika na wale wenye umuhimu kwao.
- Watoto wanahitaji kujihisi kulindwa kihisia na kimwili
- Watoto wanahitaji kuhisi wanaheshimiwa na wenzao.
- Watoto wanahitaji kujihisi kuwa ni sehemu ya makundi wanayoishi nayo.

Mahitaji ya kijamii ya watoto yakitimizwa, wanachanua kuwa watu wenye afya na mtazamo chanya wenye msimamo kwa shule na jamii zao. Wanakuwa wanafunzi wazuri na kuwekeza vipaji na nguvu zao kwa maendeleo ya wote.

Mahitaji yao ya kijamii yasipotimizwa, watoto hujihisi wana upungufu na kutumia nguvu nyingi kujaribu kufidia upungufu huu. Hivyo tunawakuta wanafunzi wenye akili wakifanya chaguzi mbaya, au kushindwa kuhimili misukumo ya rika lao wakati wakijua haiwasaidii na wala siyo kwa manufaa yao. Wasichana wanaweza kuwa na hatari kubwa ya kuathirika zaidi kwa kutumika vibaya kijinsia. Wakati wanachunguza nafsi zao kijamii na wakati miili yao ikibadilika, wanaweza kulengwa kwa ajili ya uonevu na udhalilishwaji wa kijinsia.

Shule bora inajitahidi kuwalinda watoto kutokana na hatari hizo kwa kutengeneza mazingira ya kijamii yanayoitikia vizuri kutimiza mahitaji ya kijamii ya watoto. Kutimiza mahitaji ya kijamii ya watoto, ili kuwawezesha kukua kijamii kunahitaji yafuatayo:

- Kuendeleza hadhi ya watoto
- Kulea sauti ya kipekee ya watoto
- Kusaidia kukuza nidhamu binafsi ya watoto.




Mahitaji ya kijamii ya watoto yakitimizwa, wanachanua kuwa watu wenye afya na mtazamo chanya. Wanagundua sauti yao, wanapata ufahamu wa utu wao kama mtu mmoja mmoja na kukuza nidhamu binafsi katika mchakato wao wa kujifunza.

## Hadhi

Watoto wana hisia teke kuhusu hadhi yao. Wanawatazama watu wazima muhimu katika maisha yao kuwahakikishia kuwa wao wanastahili kuheshimiwa na kupewa staha kama watu. Wanatafuta kuhakikishiwa hali hiyo katika mahusiano yao, katika kanuni na mipangilio ya mazingira yao na katika majibu wanayoyaomba kwa michango wanayotoa katika mazingira yao.

Hadhi ya mtu ni imani ya msingi kwamba thamani yake kama mtu haiwezi kupunguzwa na kwamba thamani yake haina masharti. Watu wenye hisia bora ya hadhi wanajivunia walivyo na wanavyohusiana na wenzao na mazingira.

Imani ya watoto katika hadhi yao haijitokezi yenyewe tu, bali hupaliliwa kwa muda kwa njia mbalimbali. Kama watu wazima, tunaweza kulea hisia za hadhi ya watoto kwa kuwafanya wahisi mahusiano yanayoendeleza; kwa kuwaongoza na kuwapa mfano mzuri wa maadili na tabia; kwa kuwasaidia kukubali kuwajibika kwa mawazo na vitendo vyao; Kwa kuweka mazingira thabiti ya heshima ambamo watoto wanaweza kuchunguza utambulisho wao.

Watoto wakizoea kuwa katika mazingira haya ya elimu, watajifunza kuwa shule na jamii yao inathamini michango yao na kuwaona wao kama wanaostahili heshima.

*Watoto wanawatazama watu wazima katika maisha yao kujihakikishia kuwa wanastahili kuheshimiwa na kupewa staha kama watu.*

# Shule zinazoheshimu hadhi ya watoto ni pamoja na:

## Shule zinazosisimua na kutunzwa vizuri

Shule inaweza kutunza na kupamba madarasa na mazingira yake kuchochea ubunifu wa watoto. Kwa kusisitiza vitu kama usafi, madarasa ya kuchora na kuonyesha kazi za sanaa za watoto, shule inawapa watoto ishara kuwa wao ni wa pekee na muhimu.

## Shule zinazojali afya

Shule inaweza kuwa na vyoo visafi na vilivyotengwa kwa matumizi ya jinsia tofauti na kuwa na vifaa vya kutosha vya usafi ili kutokuwafanya watoto kujifaragua. Hii itahusisha kuwahudumia au kuwa na mipango ya dharura kwa wsichana wanaopata hedhi. Shule inayojali afya inawasadia watoto kuwa wa kuheshimika.

## Shule isiyo na ukatili

Shele inaweza kutunga sera na mifumo inayowalinda watoto dhidi ya tabia chafu, kama uonevu na unyanyasaji wa kijinsia, hasa hasa dhidi wa watoto wa kike. Hatua hizi zinatuma ujumbe ulio wazi kwa wanafunzi kuwa shule inawathamini na haitavumilia wao kufanywa wahanga.



## Shule inayojivunia

Shule inaweza kusisitiza taswira yake chanya, kuwafanya watoto kujivunia kuwa sehemu yake. Mambo mbalimbali kama kutengeneza kwa pamoja wito wa shule au kuchora kwa pamoja ukuta unaotangaza maadili bora, yanaweza kukuza hisia za kujivuna katika utambulisho wa shule na kutengeneza wajibu wa pamoja kuhusu jinsi shule inavyoonekana nje na ndani.

*Hatua hizi zinatuma ujumbe ulio wazi kwa wanafunzi kuwa shule inawathamini na haitavumilia wao kufanywa wahanga.*

# Sauti

Sauti ya mtoto ni kielelezo chake cha pekee cha mitazamo, vipaumbele na uzoefu. Wakipewa fursa ya kukuza na kutumia sauti zao, watoto watawasilisha kwa wengine jinsi wanavyoielewa dunia na mambo gani ni muhimu kwao. Katika kukuza sauti zao wanagundua kielelezo chao wenyewe.

Sauti ni zana muhimu sana kushiriki katika michakato inayotuathiri sisi kama watu. Shule ina wajibu wa kupalilia sauti ya kila mtoto, ili mawazo ya watoto yachangie dira ya pamoja ya jinsi jamii yetu inavyopaswa kuwa. Kama sauti za watoto hazitathaminiwa au kupewa uzito unaopaswa, watoto hujifunza kuwa kimya, na kuacha mambo yao kwa jamii yao. Wanajiweka katika mtazamo kuwa hakuna wanachofikiria, kusema au kutenda kina maana. Imani hii hukuza hali ya kutojali na kujitoa katika michakato ya jamii, ambayo inaweza kuwa na athari za muda mrefu kwa watoto, shule zao na nchi yao.

Shule bora inakuza sauti za kusisimua na za asili ndani ya wanafunzi wake. Inawatia moyo watoto kuchunguza mitazamo yao; Inawapa fursa watoto kugundua na kuelezea wanavyojihisi na kufikiri kuhusiana na mambo yanayowaathiri. Ni katika hali hiyo tu mawazo ya asili yanatoka. Ukosefu wa sauti za kipekee inaonyesha kudumaa na kuoza katika mfumo wowote na inabashiri kwa uhakika kuanguka kwa shule. Kama shule inatamani kustawi na kufanya vizuri, lazima iweke nafasi ya kutosha kwa fikra mbalimbali na uchunguzi wa mawazo mpya. Shule bora inatambua kuwa uwekezaji katika kuendeleza sauti zilizokomaa kuelezea maoni tofauti unachangia sana katika kutengeneza demokrasia imara na mfumo bora wa utawala.

## Shule zinazoendeleza sauti za watoto ni pamoja na:

### Shule zinazowashirikisha watoto katika kufanya maamuzi

Shule inaweza kubuni fursa kwa watoto kutoa maoni yao kwa njia inayofaa kwa kuwafanya kuwa sehemu ya mchakato wa ufanyaji maamuzi ya shule. Shule inaweza kuweka utaratibu muafaka, kama vile Mabaraza ya Wanafunzi au kamati zingine ambazo kupitia huko watoto wanaweza kugundua sauti zao na kuwa na ushawishi halisi.

## Shule zinazotia moyo utoaji wa maoni

Shule inaweza kuwekeza katika fursa kama kijarida cha shule, mashindano ya mwaka ya uandishi wa insha, michezo ya kuigiza, drama chini ya uongozi wa wanafunzi, darasa la ngoma au matukio ya michezo kuwawezesha wanafunzi kuchunguza mambo mbalimbali kuhusu wao.

## Shule zinazozingatia maoni ya wanafunzi

Shule inaweza kuwapa wanafunzi uzoefu wa mawazo yao kuzingatiwa na kusababisha mabadiliko chanya. Uzoefu huu unaweza kuhusisha kujenga hali inayovumilia maoni yanayotofautiana, pengine, kutumia ubao wa matangazo au masanduku ya maoni; kisha kutekeleza baadhi ya mapendekezo kutoka kwa wanafunzi; na hatimaye kuingia katika majadiliano na wanafunzi kuhusu kwanini maamuzi fulani yalifanyika.

## Shule zinazowafundisha wanafunzi stadi zinazosaidia ushiriki

Shule inaweza kuwasaidia wanafunzi kukuza sauti zao kwa kujenga uwezo wa wanafunzi kukosoa kwa heshima mitazamo inayotofautiana na yao na kushawishi kwa ufanisi kwa kutumia hoja nzito.



## Nidhamu Chanya

Shule bora inatumia mtazamo wa nidhamu chanya, inawapa wanafunzi mfumo unaowasaidia kufanikiwa na kukua wakati wanajifunza tabia bora na zinazokubalika kijamii. Mfumo huu unajengwa na huruma na kupata dira yake kutoka kwenye imani kwamba watoto wanahitaji kuongozwa, siyo kuadhibiwa. Katika mfumo huu, makosa ni fursa ya kufundisha badala ya kudhalilisha.

Mtazamo wa nidhamu chanya huongoza tabia za watoto kwa kulenga makuzi ya ujumla ya mtoto. Kupitia mifano mizuri, ushauri nasaha na kutoa miongozo ya wazi ya tabia zinazokubalika, inatazamia kujenga ndani ya watoto stadi na mfumo wa maadili utakaowachochea kuendeleza nidhamu chanya, kujiheshimu na uimara wa silika.

Shule bora haikimbilii kuwadhalilisha watoto kwa adhabu ya viboko. Badala yake huwasaidia watoto kujenga nidhamu kupitia ushauri nasaha, kuwapa miongozo ya wazi na kuwapa msaada endelevu. Shule bora huwasaidia watoto kujiwekea malengo kamili kwa ajili yao na kuwasaidia kujenga stadi na tabia/silika za kufikia malengo hayo. Inawapa watoto msukumo wa kushikilia malengo yao na kufahamu kuwa kufikia malengo mazuri yahitaji kufanya kazi kwa bidii.

Mtazamo wa nidhamu chanya inamlenga mtoto, kuweka mbele katika kila miingiliano maslahi mazuri ya mtoto. Ni uwekezaji wa muda mrefu katika makuzi ya mtoto, badala ya kushilia utiifu wa sasa na faida za muda mfupi.

Zana ya muhimu sana ya mtazamo huu ni uhusiano kati ya mwalimu na mtoto – sauti yake, asili yake na huruma na heshima ndani yake. Waalimu wanalea mahusiano haya katika misingi ya uelewa wao wa mahitaji ya makuzi ya mtoto na kupangilia mwitikio wao kwa watoto kwa lengo la kuwasadia wajifunze na kukua. Mtazamo huu unakumbatia nafasi ya mwalimu kama mshauri na kiongozi. Shule bora inafahamu kuwa huu uhusiano ni muhimu kwa makuzi ya mtoto, na kwa hiyo, huwekeza katika kutimiza wajibu huu kwa juhudi na hekima.

*Shule bora haikimbilii kuwadhalilisha watoto kwa adhabu ya viboko.*

# Shule zinazofanikiwa kuchukua mtazamo wa nidhamu chanya ni pamoja na:

## Shule zinazoipa nidhamu maana mpya baada ya tafakuri na mazungumzo

Shule inaweza kuanza tafakari ya pamoja juu ya mtazamo wake wa sasa kuhusu nidhamu, kuchunguza sababu za mtazamo huu kutumika na mapungufu yake. Wakati huo huo, kuanza kujifunza kuhusu mtazamo wa nidhamu chanya, faida zake na namna itakavyoletwa shuleni. Takari na mazungumzo ya ndani yakishafanyika, shule inaweza kuwapa wadau dira mbadala ya namna ya kuhusiana na watoto. Kwa kubadilishana ufahamu na mifano yao kwa kujiamini, wanachama wa shule wanaweza kuwashawishi wadau kuwa adhabu ya viboko haina nafasi katika shule bora.

## Shule zinazoendesha vizuri mpito kuelekea nidhamu chanya

Shule lazima itambue kuwa mpito kuelekea nidhamu chanya huchukua muda na kuhusisha mchakato wa kujifunza kwa waalimu na wanafunzi. Kuendeleza msimamo usioyumba wakati huu wa mpito, shule inaweza kuweka sera ya kutokuvumilia kabisa adhabu ya viboko na kutunga sera ya nidhamu iliyoandikwa (Tazama ukurusa wa 37).

## Shule zinazojenga uwezo wa waalimu wake kutumia mikakati ya nidhanmu chanya.

Shule lazima zitoe nafasi mara kwa mara kwa waalimu kujifunza na kufanyia mazoezi njia mbadala za kuwafundisha watoto nidhamu. Mtazamo wa nidhamu chanya unatumia mikakati kama wa kushirikiana na watoto kuweka nidhamu kwa pamoja.

Kushirikiana na watoto kuweka nidhamu kwa pamoja inajumuisha yafuatayo:

- Uundaji wa kamati za nidhamu za darasa inayoshiriki katika kuweka nidhamu.
- Kuweka kanuni na malengo ya darasa kwa pamoja.
- Fursa kwa wanafunzi kutafakari na kueleza kwa ufasaha jinsi tabia fulani zinavyotatiza
- Fursa kwa wanafunzi kutafakari na kushirikishana uchaguzi wa tabia mbadala.

Kwa ushauri wa ziada wa kufaa, tafadhali tazama chapisho mwenza inayojielekeza katika kusaidia nidhamu chanya shuleni[5], inayopatikana Raising Voices kwenye tovuti www.raisingvoices.org.



*Ukuaji kimaadili unastawishwa na kulelewa kwa maelekezo ya wazi kuhusu tabia gani inakubalika, ipi haikubaliki na kwa nini ni hivyo.*

# Sura ya 4 | Ukuaji wa Maadili katika Shule Bora

*Jinsi tunavyokusanya uzoefu, kila mmoja wetu anajaribu kuendeleza viwango vya mfumo ambao utakuwa dira yetu ya maadili. Tunavyochangamana na dunia, tunajaribu tunayoyaamini, yanayotufaa na jinsi gani tunaamua kitu kizuri kutoka kwenye kibaya. Hatimaye, mwelekeo wa imani tunayoichukua, jinsi gani tunaishika kwa makini na uaminifu, kiasi gani tutafanikiwa kufikia katika maisha yetu, ndiyo itakayoamua kitu gani tutakuwa humu duniani.*

Shule zina ushawishi mkubwa kwenye ukuaji wa maadili kwa watoto. Mamabo wanayoshuhudia watoto, wanayojifunza na kuweka akilini, wanayoshiriki kufanya huja kuwa malighafi kwa utambulisho wao wa kimaadili. Wanaangalia kitu gani shule inatangaza kuhusu thamani ya mtu; wanashuhudia jinsi haki inavyoendeshwa; wanazingatia viwango vinavyowekwa na kushikiliwa na shule; wanajifunza mambo ya kina kuhusu jinsi uhalisia unavyofanya kazi katika dunia wanayoanza kuigundua tu sasa.

Kwa watoto wengi, shule ni mazingira ya kwanza wanayokutana nayo nje ya familia zao. Hivyo, watoto wanatazamia shule kufidia mapungufu yaliyoachwa na mazingira ya nyumbani, kusuluhisha migogoro waliyoyapata katika mitazamao yao ya maadili. Kama mzazi ni mkorofi au hayupo, mtoto anatazamia shule kuelewa hiyo maana yake ni nini. Kama kuna uhaba wa mawasiliano nyumbani, au kutokuwepo kwa mfumo wowote wa utambuzi kwa ajili ya kutathmini tabia inayofaa, mtoto atatafuta vipengele vinavyokosekana shuleni.


Kama shule zikishindwa kuwapa vipengele hivyo, basi watoto watajitafutia majibu yasiyopangiliwa, aghalabu kwa kuvunja mila kwa hasara kwao na jamii zao. Tabia za ukorofi, uhalifu na rushwa hazianguki kwa ghafla kutoka angani, bali ni matokeo ya mapungufu yaliyoachwa wazi katika ukuaji wa maadili ya mtu. Kwa hiyo, ni muhimu kwa shule kuwekeza katika ukuaji wa kimaadili kwa watoto.

Ukuaji kimaadili unastawishwa na kulelewa kwa maelekezo ya dhahiri kuhusu tabia zinazokubalika, zipi hazikubaliki na kwa nini. Shule bora inapalilia ukuajia maadili kwa kutoa mfano, ushauri nasaha, kuonyesha maadili kwa vitendo na kujenga uzingatiaji wahaki za binadamu. Kwa mfumo wa maadili kujijenga ndani ya mtu, mtu huyo lazima akutane na maelezo yake dhahiri, kuiona ikifanya kazi, katika muundo wa utawala na sera za mazingira yanayomzunguka na uzoefu wake unaodumu kwa muda mrefu.

Ukuaji wa maadili ni matamanio ya juu tuliyonayo kama wanadamu, na lakini ni sehemu ya maisha yetu ambayo tunapata uongozi na msaada usiotosheleza. Ni sehemu muhimu ya jinsi tunavyotenda duniani, tunayoyaona siyo sahihi na tunayoamua kuwa ya haki. Mitazamo yetu ya maadili ni ramani yetu ya kupita mitanziko tutakayokumbana nayo.

Matamanio yenye nguvu sana ambayo shule inaweza kuwajengea watoto ni kiu ya maisha yote ya kutaka kuboresha maadili yao. Katika uhalisia, shule bora inaweza kusaidia ukuaji kimaadili wa watoto kwa kuweka na kudumisha mahusiano ya madili, kuwa na viwango vinavyokubalika, sera ya kuaminika iliyoandikwa, utawala unaojali na ushiriki mpana wa jamii katika utendaji wake kimaadili.

*Shule bora inapalilia ukuaji wa maadili kupitia mahusiano yenye huruma, kutoa mifano ya kuigwa, ushauri nasaha na kuonyesha maadili kwa vitendo.*




Watoto wanapopata mahusiano yenye huruma kupitia watu wenye mwenendo mzuri wa kuigwa na washauri wenye hekima, na shule zao zikiweka mazingira yaliyapangiliwa na viwango dhahiri, watakuza mfumo wa maadili kwa maisha yao yote utakaowasaidia wao kuwa na maadili na wanajamii hai.

## Uhusiano kimaadili

Kwanza kabisa, shule lazima ipate nia dhahiri kutoka kwa wanajamii watu wazima kwamba watajitahidi kuwa na mahusiano mazuri na yanayowawezesha watoto kwa kuheshimu haki zao. Hii ina maana kwamba, kupita utambulisho wake kwa umma, na pia kupitia michakato yake ya ndani, shule lazima iwazoeshe watu wazima kuheshimu utu wa watoto, kusaidia maendeleo ya watoto na mara zote kutenda kwa maslahi ya watoto. Watu wazima lazima waonyeshe uadilifu na uaminifu wa nia zao. Lazima wawe mfano wa mfumo bora wa maadili wa pamoja kwa tabia zao na kuwashauri watoto kujenga utambulisho chanya. Watu wazima lazima walenge kuwavutia watoto kubuni uwezo mkubwa zaidi na kukuza nidhamu ili kufikia malengo yao.

Shule lazima zihakikishe kuwa waalimu hawawanyanyasi wasichana kijinsia na kuwa waalimu wanafahamu wajibu wao wa kuonyesha tabia za mfano katika kuendeleza afya ya kijinsi kwa watoto wote.

*Shule lazima ipate nia dhahiri kutoka kwa wanajamii watu wazima kwamba watajitahidi kuwa na mahusiano mazuri na yanayowawezesha watoto.*



# Viwango

Ikiwa ni pamoja na lengo la kuweka mahusiano ya kimaadili, shule lazima ziweke viwango dhahiri ambavyo kila mtu shuleni ataweka nia ya kuviendeleza. Viwango ni maadili ya msingi ambayo shule huazimia na hulenga kuyafuata. Vinaainisha matamanio ya pamoja ya shule na vimeelezwa kwa njia inayowavutia wanashule kujiwekea malengo yanayohusiana navyo na kujisukuma kuyafikia.

Shule bora inaweka kwa uaminifu viwango vyake, kama vile:

- Tunajitajihidi kuwa na nidhamu chanya katika shule yetu.
- Tunajitahidi kuheshimu utu wa kila mwanashule wetu.
- Tunasherehekea mafanikia ya kila mmoja katika shule yetu.
- Tunajivunia shule yetu na kuionyesha kwa jinsi tulivyo, kwa tabia na mazingira yetu.

Shule bora ina utamaduni wa ndani ulioelezwa vizuri unaoendeleza viwango hivi. Wanafunzi wanaonyeshwa na kuingizwa ndani ya viwango hivi kwa njia mbalimbali kila siku. Kwa shule yote kuna jitihada za pamoja za kuendeleza viwango hivi – kutoka kwenye wito wa shule na msisitizo wa kila mara kwenye mikusanyiko ya asubuhi mpaka kwenye ujumbe uliobandikwa kimkakati katika maeneo yote ya shule na tabia na vitendo vya kila mmoja shuleni.

Viwango siyo sawa na kanuni za shule. Kanuni ni miongozo halisi ya namna ya kudumisha viwango. Kwa mfano, kanuni kwamba "Uharibifu wa mali za shule hautavumiliwa" inaunga mkono kiwango "Tutajivunia mazingira yetu." Kanuni inayopiga marufuku adhabu ya viboko inaunga mkono kiwango "Tunaheshimu utu wa kila mmoja wa wanashule wetu." Kanuni bila kuwa na viwango dhahiri vilivyoelezwa vizuri zinakuwa za kidikteta na huchochea hali ya kutozijali. Viwango vinatoa msingi wa kanuni na tabia shuleni. Vinaonyesha kwa kila mmoja shuleni kwamba kanuni haziko pale kuwadhibiti wao, bali kumsaidia kila mmoja kufikia malengo yake.

*Viwango ni maadili ya msingi ambayo shule huazimia na hulenga kuyafuata.*

# Sera ya kuaminika iliyoandikwa

Viwango bila sera ya kuaminika iliyoandikwa na kuonekana ikitekelezwa huwa maneno matupu, ambayo kwayo watu hupoteza imani haraka. Shule bora hutunza kimaandishi dira yake, maadili, viwango na kanuni, pamoja na adhabu inayoendana na kwenda kinyume. Mifano ya nyaraka za sera kama hizo inajumuisha yafuatayo:

## Katiba ya Shule

Katiba ya shule inaelezea dira ya ujumla, utume na maadili ya shule na kueleza kwa kina namna gani hayo yatafikiwa. Inaeleza nani atapewa mamlaka ya kuhakikisha kuwa shule inabaki na utiifu kwa mambo yaliyomo ndani ya katiba na jinsi gani chombo hicho kitatekeleza wajibu wake.

## Kanuni za Maadili ya Waalimu

Kanuni za maadili ya walimu hueleza maadili na viwango ambavyo shule hutegemea waalimu wake kuyashika na jinsi shule itakavyowasaidia kutekeleza wajibu huu. Waraka huu pia hueleza adhabu itakayotolewa kwa kushindwa kushika majukumu haya.



## Kanuni za Maadili ya Wanafunzi

Kanuni za maadili ya wanafunzi hueleza shule inategemea nini kutoka kwa wanafunzi wake na jinsi itakavyowasaidia wanafunzi kutii viwango hivi. Waraka huu pia unaeleza vizuri adhabu kwa wanafunzi kushindwa kutimiza matarajio haya.

## Sera ya Nidhamu

Sera ya nidhamu hueleza malengo ya sera hatua mahususi zitakazochukuliwa na shule kosa linaponyika. Sera hii yapasa kuongozwa na viwango vilivyokubalika na shule na vinafuata sheria za nchi na mwongozo wowote wa sera uliotolewa na mamlaka za serikali zinazohusika. (Kwa mfano, katika nchi nyingi ambamo adhabu ya viboko imepigwa marufuku shuleni, sera ya shule haiwezi kuihalalisha.)

Sera ya nidhamu lazima itengenezwe kupitia mchakato shirikishi, ukiwaruhusu kila mmoja shuleni kujisikia alikuwa na sauti katika kutengeneza utamaduni watakaotarajiwa kuendeleza na kushika. Mchakazo huu unaweza kuhitaji kugawanywa katika hatua kadhaa, kama vile (1) mashauriano na wanashule wote, (2) kundi dogo lilikasimishwa kutengeneza rasimu ya sera, (3) mrejesho mpana wa rasimu ya sera na (4) idhini ya mwisho ya chombo cha utawala cha shule.

*Viwango bila sera iliyoandikwa huwa maneno matupu, ambayo kwayo watu hupoteza imani haraka.*

## Utawala unaowajibika

Mara shule ikikubali rasmi sera zake zilizoandikwa, wanashule wote lazima wajichukulie wajibu wa kushiriki kwa usawa utoaji na wajibu wa kuzitekeleza na wadau muhimu wote, wakiwamo watoto. Kupitia mazoea kama hayo watoto hujifunza kuwa wao pia wana nafasi ya kusema kitu gani kinatokea shuleni kwao na wajibu wa kudumisha nidhamu katika shuke yao.

Uvunjaji dhahiri wa sera usiopingwa hupunguza imani ya kila mmoja kwa sera zilizotengenezwa, ukigeuza uaminifu utakaowekwa kwake na mtu kutetea vipaumbele vyake. Sera hizi zitapoteza uwezo wa kuwavutia watu na zitakuwa haribifu, zikionyesha kuwa shule haitekelezi yale inayoyaazimia kwa umma.

*Uvunjaji dhahiri wa sera usiopingwa hupunguza imani ya kila mmoja kwa sera zilizotengenezwa.*

# Ushiriki wa jamii

Shule siyo kisiwa. Imo ndani ya jamii pana na, kwa hiyo, inaathiriwa na kuwajibika kwa jamii inayoitumikia. Shule lazima iwakilishe matarajio ya juu kabisa ya jamii na kujitahidi kuhakikisha kuwa wanajamii wanajivunia na kujihisi wamewekeza kwenye shule yao. Wanajamii, hasa hasa wazazi, lazima wajumuishwe ili maadili wanayoyapata watoto shuleni yanaendelezwa pia nyumbani. Vilevile, taasisi za jamii lazima zihusishwe na kushirikishwa katika kuendeleza dira ya shule.



Shule zinaweza kuweka fursa za kuifanya jamii kujua maadili na utamaduni wa shule. Hii inaweza kuchukua sura ya siku ya wazazi, mwaliko wa kujiunga na chombo cha utawala wa shule, kushirikishwa mara kwa mara, kama kupata barua au kuitisha mkutano unaowapasha habari wanajamii mafanikio muhimu na maendeleo ya shule. Katika jamii zingine, shule inaweza kuwaongoza wanajamii kuona umuhimu wa kuwa na uelewa bunifu zaidi wa elimu na kusoma.

*Wanajamii, hasa hasa wazazi, lazima wajumuishwe ili maadili wanayoyapata watoto shuleni yanaendelezwa pia nyumbani.*



*Kwa muda mrefu sana tumebaki kwenye kifungo cha mzunguko wa hali ngumu na umskini wa ubunifu.*

# Maneno ya Mwisho

Shule bora ni hazina ya matarajio na malengo yetu muhimu. Ni tumaini letu la kupanua fursa zetu kuvuka mipaka ya mawazo yaliyoganda. Shule bora haiwasaidii tu watoto waliopo humo bali pia jamii yote kukua, kuwa na ndoto kubwa zaidi, kubuni fursa zaidi kwa maisha yetu ya baadaye.

Kwa muda mrefu sana tumebaki kwenye kifungo cha mzunguko wa hali ngumu na umaskini wa ubunifu. Tumebaki tumetegwa pembezoni mwa uchumi wa dunia na uendeshaji wa fikra na uelekeo mpya. Kwa muda mrefu sana tumebaki kuwa wapokeaji wa vipaumbele vya wengine na waombaji kwenye midahalo ya ulimwengu. Sasa tumeshika ufunguo wa kujifungua wenyewe kutoka kwenye mnyororo huo. Swali ni kwamba, tutautumia?

# Maelezo

1) Chukua kwa mfano hali ya Uganda. Mwaka 1997, wakati UPE (Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Wote) ulipoanzishwa, wanafunzi 2,159,850 walijiandikisha darasa la 1. Kati ya wanafunzi hawa ni wanafunzi 485,703 walimaliza darasa la 7 mwaka 2003. Wakati idadi ya wanafunzi wanaobaki ni ngumu kuipata kwa usahihi, takwimu hizi zinaashiria kuwa kiwango cha wanafunzi kubaki ni kadirio la 23%. Wanafunzi wengi walioacha shule walisema "kukosa moyo wa kusoma" kama sababu yao ya msingi (46%), sababu za kifamilia (15%) na ugonjwa (12%). Tazama mjadala zaidi kuhusu hili katika Overseas Devlopment Institute: Universal Primary Education, Uganda (2006). Inapatikana kwenye tovuti: //www.odi.org.uk/interregional_inequality/papers/Policy Brief 10 –Uganda.pdf. Ilitumika Machi 10, 2007.

2) Assessment of Violence Against Children in the Eastern and Southern Africa Region. F. Zuberi, UNICEF ESARO (2005). Inapatikana kwenye tovuti www.crin.org/docs/ESA_Regional_Assessment_final.doc. Ilitumika Machi 27, 2007
Violence Against Children: The Voices of Ugandan Children and Adults. D. Naker Raising Voices (2005). Inapatikana kwenye tovuti www.raisingvoices.org. Ilitumika Machi 27, 2007

3) Imetokana na kuchukuliwa kutoka "Cognitive Learning Stages" in The Architecture of Cognition. Cambrige, Anderson J. R. (1983), MA: Havard University Press. Pia imetokana na kuchukuliwa kutoka kwenye hatua nne za kujifunza ilivyopoendekezwa na Jean Piaget.

4) Imerahisishwa na kuchukuliwa kutoka kwenye nadharia ya psychosocial development ya Erick Erickson, ambayo inasema kuwa kila mtu lazzima apitie hatua nane ya ukuaji kijamii kufikia ukomavu wa psychosocial na kwamba upitaji muafaka unategemea mazingira saidizi ya kijamii. Mawazo haya pia yameungwa mkono na kazi ya Heinz Kohut, ambayo inasema kuwa mtu anakuza uwezo kupitia mkazo wa mahusiano ya kijamii.

5) Alternative to Corporal Punishment: Promoting Positive Discipline in Our Schools. D. Naker, Raising Voices (2007). Inaptikana kwenye tovuti www.raisingvoices.org.

# Marejeo yaliyoshauriwa

1) World Report on Viloence against Children. Paulo Sergio Pinheiro. United Nation's study of violence against children (2006). Inapatikanakwenye tovuti www.violencestudy.org. Ilitumika Machi 27, 2007. Chapter 4: Violence against Children in Schools and Educational Setting may be of particular interest.

2) Millennium Development Goals (2000-2006). Inapatikana kwenye tovuti http://www.un.org/millenniumgoals/. Ilitumika Machi 27, 2007.

3) Education for All. A framework for Action in Sub Saharan Africa: Education for African Renaissance in the Twenty-first Century. Inapatikana kwenye tovuti http://unesdoc.unesco.org/images/0012/001211/121147 e.pdf. Ilitumika Machi 27, 2007.

4) EFA Global Monitoring Report 2005: The Quality Imperative. UNESCO (2004). Inapatikana kwenye tovuti www.efareport.unesco.org Ilitumika Machi 27, 2007.

## Ideas

## Ideas

Kile anachokitaka mzazi bora na mwenye busara kwa mtoto wake mwenyewe; hicho lazima kiwe hitaji la jamii kwa watoto wake.

*John Dewey*




Raising Voices

*16 Tufnell Drive*
*Kamwokya*
*P O Box 6770*
*Kampala, Uganda*

*Tel: +256 41 4531186*
*Fax: +256 41 4531249*
*Email: info@raisingvoices.org*
*Website: www.raisingvoices.org*